

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A
(GATCE) 2018**

650 HAIBA NA MICHEZO

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A
(GATCE) 2018**

650 HAIBA NA MICHEZO

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU
DARAJA LA A (GATCE) 2018**

650 HAIBA NA MICHEZO

Kimechapishwa na:

Baraza la Mitihani Tanzania,
P.O.Box 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2018

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI.....	iv
1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 TATHIMINI YA MAJIBU YA MTIHANI KWA KILA SWALI.....	1
2.1 SEHEMU A:	1
2.1.1 Swali .1 Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia	2
2.1.2 Swali. 2 Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia	4
2.1.3 Swali la 3:Upimaji na Tathimini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo	6
2.1.4 Swali la 4: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo	8
2.1.5 Swali la 5 Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo	9
2.1.6 Swali la 6 Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo	12
2.1.7 Swali la 7: Zana za Kufundishia na Kujifunzia	14
2.1.8 Swali la 8: Zana za Kufundishia na Kujifunzia	16
2.1.9 Swali 9. Maandalizi ya Ufundishaji, wa Somo la Haiba na Michezo.	19
2.1.10 Swali la 10 Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo	21
2.2 SEHEMU B	23
2.2.1 Swali 11 Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo	23
2.2.2 Swali 12. Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia	27
2.2.3 Swali 13 Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo	31
2.2.4 Swali 14 Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia.	36
2.2.5 Swali la 15 Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo	41
2.2.6 Swali 16 Upimaji na Tathimini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo	45
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA.....	49
4.0 HITIMISHO	50
5.0 MAPENDEKEZO.	51
KIAMBATANISHO.....	52

DIBAJI

Taarifa ya Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Haiba na Michezo Daraja la A ngazi ya cheti imetayarishwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, wakufunzi, watunga sera pamoja na wadau wengine wa elimu. Mtihani ni sehemu kigezo mojawapo cha kuwezesha kutathmini mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika kutekeleza mtaala wa ngazi husika. Mtihani wa Haiba na Michezo ngazi ya cheti utawezesha kutoa mrejesho kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo. Majibu ya watahiniwa katika mtihani huweza kuashiria viwango na ubora wa mielekeo, stadi na maarifa ambayo watahiniwa wameweza kuyapata katika kujifunza taaluma na uthalam wa kufundisha katika miaka miwili ambayo wanachuo walikuwa katika mafunzo.

Katika kufanya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, sababu zilizofanya watahiniwa kujibu maswali vizuri au kushindwa kujibu vizuri zimeainishwa. Uchambuzi wa kila mada na kiwango cha kufaulu katika mada husika pia umefanyika na sababu za mada hizo kufanyika vizuri au vibaya kubainishwa.

Uchambuzi wa majibu uliofanyika unaonesha kuwa watahiniwa waliowengi walifaulu mtihani wa somo la Haiba na Michezo kwa kiwango kizuri. Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa wengi waliofanya mtihani wa osmo la Haiba na Michezo waliweza kuelewa matakwa ya maswali ya mtihani huo na hivyo kuwawezesha kutoa majibu yaliyokidhi mahitaji ya maswali hayo. Aidha, watahiniwa pia walionesha kuwa na maarifa, stadi na mielekeo waliyotarajiwa kuwanayo ambayo imewawezesha kufanya vizuri katika mtihani wao. Pamoja na watahiniwa wengi kufanya vizuri katika mtihani wa somo la Haiba na Michezo, wapo watahiniwa wachache walio shindwa kujibu vizuri baadhi ya maswali. Sababu zilizobainika kusababisha watahiniwa hao kushindwa kujibu maswali kwa ufasaha ni pamoja na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika, kutoelewa matakwa ya maswali na hivyo kutoa majibu ambayo hayakujibu maswali yaliyoulizwa, kutokuwa makini katika kusoma maswali hivyo kuwafanya watoe majibu ambayo hayakuendana na matakwa ya maswali.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, taarifa hii itatoa mrejesho ambaou utatumia na wadau mbalimbali katika kuboresha mafunzo ya somo la Haiba na Michezo katika ngazi ya cheti na pia kushughulikia kasoro zilizobainishwa ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vya Elimu na hivyo, kuwezesha kutoa walimu bora wa somo la Haiba na Michezo na kuboresha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa tarajali.



Dkt. Charles E. Msonde
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Ualimu Daraja la A mwaka 2018 kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa somo la Haiba na Michezo.

Maswali ya mtihani wa somo la Haiba na Michezo yalitokana na mada tano zinazofundishwa katika ngazi ya cheti. Mtihani wa somo la Haiba na Michezo ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyogawanywa katika sehemu A na B. watahiniwa walitakiwa kujibu maswali kumi na nne (14) ambapo sehemu A walitakiwa kujibu maswali yote kumi (10). Sehemu B ilikuwa na maswali sita (6) ya insha, mtahiniwa alitakiwa kuchagua na kujibu maswali manne (4) kutoka sehemu hii.

Jumla ya 4,900 walisajiliwa kufanya mtihani wa somo la Haiba na Michezo. Kati yao, watahiniwa 4,843 sawa na asilimia 98.7 walifanya mtihani huo. Kiwango cha ufaulu katika mtihani huo kilikuwa kizuri kwani asilimia 99.88 ya watahiniwa wote walifanya mtihani huo walifaulu. Aidha, ni asilimia 0.2 tu ndiyo hawakumudu kufaulu katika kiwango cha kuridhisha.

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika makundi matatu, ambayo ni ufaulu hafifu, ufaulu wa wastani na ufaulu mzuri kutegemea alama walizopata watahiniwa katika swali. Aidha, sababu za watahiniwa kujibu swali vizuri au kushindwa kujibu zimeainishwa. Ili kuthibitisha sababu hizo, sampuli za majibu ya watahiniwa zimetumika kama vielelezo ili kuwezesha wadau mbalimbali kuona mifano ya hoja zinazotolewa.


2.0 TATHIMINI YA MAJIBU YA MTIHANI KWA KILA SWALI

2.1 SEHEMU A:

Sehemu A ya mtihani wa somo la Haiba na Michezo ilikuwa na jumla ya maswali 10 ya majibu mafupi. Kila swali katika sehemu hiyo lilikuwa na jumla ya alama nne (4). Kufaulu kwa watahiniwa katika sehemu hii kuligawanywa katika makundi matatu kulingana na alama walizopata watahiniwa. Watahiniwa waliopata alama kati ya 0 hadi 1.5 walihesabika kuwa na ufaulu hafifu katika swali husika. Watahiniwa walihesabika kuwa na ufaulu wa wastani iwapo walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 na walihesabika kuwa na ufaulu mzuri iwapo walipata kati ya alama 3 hadi 4.

2.1.1 Swali la 1: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia.

Swali la 1 lilitoka katika mada ya Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia. Swali lililenga kupima ufaamu wa watahiniwa kuhusu vipengele vya muhtasari wa somo la Haiba na Michezo. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walifanya swali hilo. Kati ya hao, watahiniwa 569 (11.7%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 922 (19.0%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambaao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 3,352 (69.3%) walipata alama kati ya 3 hadi 4 ambaao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifaalu swali hili kwa kiwango kizuri kutokana na jumla ya watahiniwa 4,274 (88.3%) kupata kati ya alama 2 hadi 4 ambazo ndizo alama zilizowawezesha kufaulu swali hili.



Chati Na. 1: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 1

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufaamu mzuri kuhusu vipengele vya muhtasari wa somo la Haiba na Michezo suala ambalo liliwawezesha kujibu swali hili kwa ufasaha. Sababu za watahiniwa kujibu vizuri ni kutokana na kuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa waliweza kuchanganua vipengele vya muhtasari kama vile mada kuu, mada ndogo, mbinu za kufundishia na kujifunzia, malengo makuu na mahususi. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi na kupata alama zote.

Kielelezo Na. 1.1

1.	Vipengele vya Muhtasari wa Haiba na Michezo ni kama vifaa tangu:
i)	Mada kuu na nafago, hiki ni kipengele Mofawapo ambayo Kinaonesha Nadi kuu na jidago zilizopo kwenye Muhtasari wa Haiba na Michezo
ii)	Mbinu za kufundishia na kujifunza, ni kipengele ambaebo Kinaonesha Ndi, u zidi zitumika kufundishia Nadi futuni ya Haiba na Michezo
iii)	Zana za kufundishia na kujifunza, bapa huainiziwa zina Nbalimbedi ambazo zinazua kuruoniwa wakati wa Ufundishaji na Ujifunzaji wa Nadi futuni.
iv)	Malengo Nakuu na Mahusici ya Somo, katika kipengele hiki huonesha Matarajio ambayo yanatakiwa kufikia na katiha pipinchi fulani.

Kielelezo Na. 1.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliywenza kueleza kwa kifupi vipengele vya muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.

Hata hivyo, ufaulu wa watahiniwa 569 (11.7%) ulikuwa hafifu. Ufaulu huu hafifu unahuishwa na baadhi ya watahiniwa kuchanganua vipengele vichache vya muhtasari. Kwa mfano, kutaja vipengele viwili badala ya vipengele vinne, baadhi ya hoja kukosa ufanuzi fasaha na kuandika majibu ambayo hayalengi kujibu swali husika, kutokuelewa matakwa ya swali hivyo, kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika muundo wa muhtasari badala ya kutaja vipengele vya muhtasari. Kielelezo Na.1.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vibaya na kukosa alama zote.


Kielelezo Na. 1.2

oi	z Utangulizi; Katika kipengele hiki waneeleza ku-judia la muhtasari.
ii	Malengo; Katika kipengele hiki waneeonesha.
iii	Malengo Matarajio ya muhtasari
iv	yalijomo
v	Maudhui

Kielelezo Na. 1.2: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa kifupi vipengele vya muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.

2.1.2 Swali la 2: Maandalizi ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia.

Swali la 2 lilitoka katika mada ya Maandiko, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia. Swali lilenga kupima ufahamu wa mtahiniwa kuhusu tofauti kati ya kitabu cha kiada na kitabu cha ziada. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kueleza kwa kifupi tofauti nne kati ya kitabu cha kiada na kitabu cha ziada. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walifanya swali hilo. Kati ya hao, watahiniwa 135 (2.8%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 148 (3.1%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambaao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 4,560 (94.1%) walipata alama kati ya 3 hadi 4 ambaao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifaalu swali hili kwa kiwango kizuri kutokana na watahiniwa 4,708 (97.2%) kupata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ndizo alama zilizowawezesha kufaulu swali hili.



Chati Na. 2: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 2

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hilo unaonesha kuwa watahiniwa walio wengi walikuwa na ufahamu kuhusu kitabu cha kiada na kitabu cha ziada suala ambalo liliwezesha kujibu swali hili kwa ufasaha. Sababu ya watahiniwa kujibu swali hili vizuri ni kutokana na kuwa na uelewa wa matakwa ya swali na hivyo kuweza kueleza tofauti kati ya kitabu cha kiada na kitabu cha ziada kama vile, kitabu cha kiada hutumiika kufundishia darasani wakati kitabu cha ziada hutumiwa muda wa ziada kama rejea. Pia kitabu cha kiada huendana na muhtasari wa somo wakati kitabu cha ziada kinawenza kuwa na baadhi tu ya mada zilizopo kwenye

muhtasari wa somo. Ufaulu huu mzuri, pia unahusishwa na uelewa wa watahiniwa katika mada hii wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri na kupata alama zote.

Kielelezo Na. 2.1

02.	Kitabu cha krada	Kitabu cha erada
	✓ ni kitabu ambacho hutumi - humusi na muhalimi na mwa na muhalimi na mwanaunganuzi. Lakini hakuna funzi chenye mtririsko wa mtririsko mewi wa mada. krada	✓ Hutumika kufundishe na - hutumika kua muda wa kujiunza darasani erada
	✓ kitabu cha krada kinae - hakserdani na muhtasari ordana na muhtasari wa mada somo la Hasba na kiche somo hujisla	✓ mada
	✓ kinapuata infumo rasi ni - hakipuati infumo rasi ni hivyo hutumika kama rejea tu	

Kielelezo Na. 2.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza tofauti kati ya kitabu cha ziada na kitabu cha kiada kwa kifupi.

Licha ya watahiniwa wengi kupata ufaulu mzuri, watahiniwa 135 (2.8%) walikuwa na ufaulu hafifu. Ufaulu huu ulichangiwa na baadhi ya watahiniwa kukosa maarifa mbayo yangewawezesha kutoa majibu yaliyokusudiwa na hivyo kuandika majibu ambayo hayakuwa sahihi. Kama kielelezo Na. 2.2 kinavyoonesha.


Kielelezo Na. 2.2

.	ziada,	ziada,
ni kitabu ambacho -	M kitabu ambacho kine nafunio	
kinetumivu na	ne mwanefuni latika ujifunzaji	
muhalimi,		
M kitabu ambacho	M kitabu ambacho kine marwei	
hekiu marwei yekunefuni	y - mwanefuni latika kujifunzo.	

Kielelezo Na. 2.2: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza tofauti nne kati ya kitabu cha kiada na kitabu cha ziada.

2.1.3 Swali la 3: Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali la 3 lilitoka katika mada ya Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo. Swali lililenga kupima ufaamu wa watahiniwa kuhusu zana za upimaji zinazotumika kupima ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kubainisha aina nne za zana za upimaji. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walifanya swali hili. Kati ya hao, watahiniwa 405 (8.4%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 488 (10.0%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambaao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 3,950 (81.6%) walipata kati ya alama 3 hadi 4 ambaao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaalu swali hili kwa kiwango kizuri kutokana na watahiniwa 4,438 (91.7%) kupata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ndizo alama zilizowawezesha kufaulu swali hili



Chati Na. 3: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 3

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufaamu mzuri kuhusu zana za upimaji zinazotumika kupima ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo suala ambalo liliwawezesha kujibu swali kwa ufasaha. Ufaulu huu mzuri unahuishwa pia na sababu mbali mbali, zikiwemo; watahiniwa kuelewa matakwa ya swali na pia kuwa na maarifa yanayotakiwa kuhusu zana za upimaji zinazotumika kupima ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa waliweza kueleza aina nne za zana za upimaji zinazotumika kupima ufundishaji na ujifunzaji kama vile maswali dodoso, mkoba wa kazi, orodha hakiki, mitihani na majaribio. Kielelezo Na.1.5 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali la tatu na kupata alama zote.

Kielelezo Na. 3.1

3	Mitihani majibio na marosai, mitolewa kota baada ya wice, kisaidi na muthila.
3	b) Mikota wa kasi, ni mkuanyiko wa nyaraka mba limbalii ginoohuu upima ujifunzaji na ufundishi Shajii
3	c) Orochha hakiki, ni orochha inayotumika katika suala lai upimaji
3	d) Majonzi ciidaro ni mawali ya kustafuta kupi a kuhusu mimo fulani.

Kielelezo Na. 3.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeeweza kueleza kwa kifupi aina nne ya zana za upimaji zinazotumika kupima ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.


Hata hivyo, pamoja na watahiniwa wengi kupata ufaulu mzuri, watahiniwa 405 (8.4%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 amba ni ufaulu hafifu. Ufaulu huu unahuishwa na baadhi ya watahiniwa kutokuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, wapo watahiniwa walioandika aina za upimaji, badala ya kuandika aina za zana za upimaji. Kielelezo Na.1.6 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vibaya na hivyo kutopata alama.

3.	Kuelere kwa kijusi, aina nne za upimaji zinazotumika kupima ujundishaji na ujifunzaji. Upimaji awali: hii ni aina ya upimaji gizambaro luyanya wa kujisia mafanikia aliyejibayo mimi kablaya i kuanza majunzo jutani. Upimaji endelekutu Ni aina ya upimaji ambayo inayantika wakati mchakato wa ujundishaji unaendeleo i nyayo zozeti majaribio na mitihani. Upimaji tatuizi: pia hii ni aina ya upimaji ambayo huwa na lengo la katali matatizo mbaalimbati katiwa ujifunzaji. Upimaji tamali: Ni aina ya upimaji ambayo luyanya wa Marishoni Mwanzo Mafanikia kwa ngezi fulani nyani kideko cha mme, nitibao wa Taabi.
----	---

Kielelezo Na. 3.2: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyechanganya dhana ya aina za upimaji na dhana ya aina ya zana za upimaji, hivyo hakupata alama zozote.

2.1.4 Swali la 4: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali la 4 lilitoka katika mada ya Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo. Swali lililenga kupima ufahamu wa watahiniwa kuhusu njia zinazochochea ari ya kujifunza kwa wanafunzi tofauti. Mtahiniwa alitakiwa achanganue njia nne zinazochochea ari ya kujifunza kwa wanafunzi wenyewe tabia tofauti. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walifanya swali hili. Kati ya hao, watahiniwa 1,732 (35.8%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 1,787 (36.9%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambaao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 1,324 (27.3%) walipata kati ya alama 3 hadi 4 ambaao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaalu swali hili kwa kiwango cha wastani kutokana na watahiniwa 3,111 (64.2%) kati ya watahiniwa 4,843 (100%) kupata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ndizo alama zilizowawezesha kufaulu swali hili.



Chati Na.4: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 4

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu kuhusu njia zinazochochea ari ya kujifunza kwa wanafunzi wenyewe tabia tofauti suala ambalo liliwawezesha kujibu swali hilo kwa ufasaha. Sababu ya watahiniwa kujibu vizuri swali hili ni kutokana na kuelewa matakwa ya swali na kuthibitisha kuwa kipengele hiki cha mada kilieleweka wakati wa mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji. Watahiniwa waliweza kuchanganua njia nne zinazo chochea ari ya kujifunza kwa wanafunzi wenyewe tabia tofauti kama vile kuwapa fursa ya kueleza mambo yanayowakabili, kuwapa zawadi wanapofanya vizuri, kuwashirikisha wakati wa kujifunza, na kuwapa maswali yanayochochea hamasa ya kujifunza. Kielelezo Na. 4.1 Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali la nne vizuri na kupata alama zote.

Kielelezo Na. 4.1

04.	Njia nne za kuchochea ari ya kujifunza Kuwa wanajunzi wenye tabia tofauti:
(i)	Kumapa motisha walijanya viuri
(ii)	Kuonyesha upendo ne kiume hanbu na
(iii)	Kumia mogo wa kuperende kusoma
(iv)	Kumapa mazoezi mengi

Kielelezo Na. 4.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliywewza kuchanganua njia nne zinazochochea ari ya kujifunza kwa wanafunzi wenye tabia tofauti.

Aidha, watahiniwa 1,732 (35.8%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa hao walifaalu kwa kiwango hafifu kutokana na kutokuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kielelezo Na.4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali la nne vibaya na kukosa alama zote.

Kielelezo Na. 4.2


4.	Njia nne zinazochochea ari ya kujifunza kwa wanafunzi wenye tabia tofauti:
i/	Njia ya Zaria
ii/	Njia ya Kuarika ugoni
iii/	Njia ya ilaswali na majibu
iv/	Njia ya Majaditino

Kielelezo Na. 4.2: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuchanganua njia zinazochochea ari ya kujifunza kwa wanafunzi wenye tabia tofauti.

2.1.5 Swali la 5: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali la 5 lilitoka katika mada ya Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kueleza kwa kifupi stadi nne za maisha ambazo mwanafunzi anajengewa kwa kusoma somo la Haiba na Michezo. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walifanya swali hili. Kati ya watahiniwa hao, watahiniwa 1,665 (34.4%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 887

(18.3%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 2,291 (47.3%) walipata alama kati ya 3 hadi 4 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifaalu swali hili kwa kiwango cha wastani kutokana na watahiniwa 3,178 (65.6%) kupata kati ya alama 2 hadi 4 ambazo ndizo alama zilizowawezesha kufaulu swali hili.



Chati Na. 5: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 5

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonyesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu wa stadi za maisha ambazo mwanafunzi anajengewa kwa kusoma somo la Haiba na Michezo na hivyo kutoa majibu sahihi. Sababu ya wanafunzi kujibu vizuri ni kutokana na kuelewa matakwa ya swali pamoja na kuwa na maarifa ya stadi anazopata mwanafunzi kwa kujifunza somo la Haiba na Michezo na hivyo kuthibitisha kuwa mada ya Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji ilieleweka wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa waliweza kueleza kwa kifupi stadi nne za maisha ambazo mwanafunzi anajengewa kwa kusoma somo la Haiba na Michezo kama vile, mawasiliano, kujiamini, kuthubutu na ushirikiano. Kielelezo Na.5.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote

Kielelezo Na. 5.1

5.	Zifurato ni stadi za maisha ambazo - mwanafunzi anajengewa kwa kusoma somo la Haiba na Michezo.
	i). stadi ya kujiamini - Mwakini anapaswa kumipa ngofisi mwanafunzi ya kujietera na kuheshimi mawazo yako ili Kunyengesa mwanafunzi hali ya kujecuni.
	ii). stadi ya mawasiliano - Mwakini anapaswa kuwashinikisha wanafunzi katika nichero ili kuwafanya wawazo kuwasiliana na kubadilishana mawazo
	iii). stadi ya kuthibutu. - Mwakini anapaswa kuchumba njia shinkisha eki katika tendu la ufuno nayo na ujifunzo ili kumuwesha mwanafunzi kushinku kwa kujibu au kumtazia mawali olarasani.
	iv). stadi ya kushinkisau ushinkiano. - Mwakini anapaswa kuwapa <u>uaitoto nefasi</u> ya kushinkia katika kujifunzo kwa kuwapa katika;

Kielelezo Na. 5.1: Kielelezo kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza stadi nne za maisha ambazo mwanafunzi anajengewa kwa kusoma somo la Haiba na Michezo

Pamoja na watahiniwa wengi kujibu swali kwa kiwango kizuri, watahiniwa 1,732 (35.8%) walijibu swali kwa kiwango hafifu na kupata ufaulu hafifu katika swali hili kutohana na baadhi ya watahiniwa kutokuelewa matakwa ya swali na kutokuwa makini wakati wa kusoma swali na kuchanganya dhana na hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.5.2 ambayo ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyefaulu kwa kiwango hafifu katika swali hili.


Kielelezo Na. 5.2

5	b) Kusoma na mwenendo na tafuta nseuri.
ii)	Tafuta stadi za maisha,
iii)	tayu kanuni ng shera mtalimbalu za viti,
w)	Utenadaji teni nseuri.

Kielelezo Na. 5.2: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa kifupi stadi nne za maisha ambazo mwanafunzi anajengewa kwa kusoma somo la Haiba na Michezo.

2.1.6 Swali la 6: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali la 6 lilitoka katika mada ya Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kuchanganua mambo manne yanayoweza kuhatarisha usalama wa wachezaji wakiwa wanacheza. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walijibu swali hilo. Kati ya hao, watahiniwa 445 (9.2%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 1,086 (22.4%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa wengine 3,311 (68.4%) walipata alama kati ya 3 hadi 4 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifaalu swali hili kwa kiwango kizuri kutokana na watahiniwa 4,397 (90.8%) kupata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ndizo alama zilizowawezesha kufaulu swali hili



Chati Na. 6: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 6

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu wa mambo yanayoweza kuhatarisha usalama wa wachezaji wakiwa wanacheza na hivyo kutoa majibu sahihi. Sababu ya watahiniwa kujibu vizuri ni kutokana na kuelewa matakwa ya swali na hivyo kuthibitisha kuwa mada ya Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo ilieleweka wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa waliweza kuchanganua kwa kifupi mambo manne ambayo yanaweza kuhatarisha usalama wa wachezaji wakiwa wanacheza kama vile, ubovu wa miundombinu, kutokufuata kanuni na sheria za mchezo, matumizi yasiyo sahihi ya vifaa vya michezo na mazingira ya michezo kutokuwa safi. Kelelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote.

Kielelezo Na. 6.1

6. Mambo yanayoweza kuhatarisha usalam a wa Wachezaji wakiwa wanacheza ni;
(i) Matumizi yasiyo sahihi ya vifaa vya - michezo; ambapo wachezaji waferiweza Kuumizana wenyeule kula wenyeule.
(ii) Kutokufuata sheria na Kanuni za mche- zo; Hii pia hupelekwa wachezaji Kuumi zana wenyeule.
(iii) Ubovu wa miundombinu ya sehemu za kuchezea michezo, ambapo hupelekwa wachezaji Kuumia.
(iv) Mazingira ya michezo Kutokana wa Safi mfano, Kuwepo kula chupa zilizopasuka miba na hata plastiki mboru.

Kielelezo Na. 6.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuchanganua mambo yanayoweza kuhatarisha usalama wa wachezaji wakiwa wanacheza.

Hata hivyo, licha ya watahiniwa wengi kupata ufaulu mzuri, watahiniwa 445 (9.2%) walipata ufaulu hafifu katika swali hili. Watahiniwa hao walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na sababu mbalimbali kama vile, baadhi ya watahiniwa kutokuelewa matakwa ya swali na kutoa majibu yasiyo sahihi na watahiniwa wengine kukosa maarifa ya kujibu

swali hili. Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya jibu baya la mtahiniwa kwa swali hili.


Kielelezo Na. 6.2

6.	(i) Kuunji ka viungo
	- Kuwa kuanguka kueenge mashimo au kuumiziwa, a watati wa michezo.
	(ii) Kuislwa pumzi na kudhiraizirai
	- Hii ni pamoja na kuchero nuda mrefu
	(iii) Migogore, na vurugu
	- Hapa ni pale ambapo kutoatuvego na maele wano tofauti vaina ya wacheraji au muendesha michezo na wacheraji
	(iv) Magonjwa (kuambukizana magonjwa).
	- Hapa ni pale ambapo wacheraji kuvwezeri kubadilishana sare za michezo na hivyo kuvaze kuse babishera muaambukizo ya magonjwa baina ya wacheraji

Kielelezo Na. 6.2: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi na kukosa alama zote.

2.1.7 Swali la 7: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali la.7 lilitoka katika mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kufafanua stadi nne muhimu anazotakiwa kuwa nazo mwalimu wa somo la Haiba na Michezo ili kumwezesha kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia papo kwa papo. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walifanya swali hili. Kati ya hao, watahiniwa 4,125 (85.2%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 213 (4.4%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambaao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 505 (10.4%) walipata alama kati ya 3 hadi 4 ambaao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walipata ufaulu hafifu katika swali hili kutokana na watahiniwa 4,125 (85.2%) kupata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambazo ziliwafanya kufaulu kwa kiwango hafifu katika swali hili



Chati Na. 7: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swalii la 7

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika hili unaonesha kuwa watahiniwa wengi hawakuwa na ufahamu wa stadi anazotakiwa kuwa nazo mwalimu wa somo la Haiba na Michezo ili kumwezesha kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia papo kwa papo hivyo kushindwa kutoa jibu sahihi. Watahiniwa wengi waliandika stadi za maisha kama vile, kujiamini kuwa na upendo, kushirikiana na kuvumilia badala ya stadi za kufaragua zana kama vile, stadi ya maandishi rahisi, uchoraji rahisi, utumiaji wa rangi, uumbaji wa maumbo rahisi, uchongaji wa maumbo rahisi kama vile, vigoda, stenseli, mihuri na kukata na kubandika maumbo rahisi. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyebainisha mambo ya kuzingatia wakati wa kufaragua zana badala ya stadi zinazomwezesha mwalimu kufaragua zana.

Kielelezo Na. 7.1

7.	i/ Afahamu umri na kuelwa wa walengwazi.
	ii/ Azingatia maelekeu anayo fundisha.
	iii/ Maizingira aliyo nazo.
	iv/ Mpangilio wa darasa lake.

Kielelezo Na. 7.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali na akatoa majibu yasiyo sahihi.

Pamoja na watahiniwa wengi kutokuwa na ufaulu mzuri katika swali hili, watahiniwa 718 (10.4%) walifaulu vizuri swali hilo. Ufaulu huu unahuishwa na sababu mbalimbali kama vile baadhi ya watahiniwa kuelewa matakwa ya swali na kutoa majibu sahihi na kuwa na maarifa kuhusu stadi za kumwezesha mwalimu wa somo la Haiba na Michezo

kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia papo kwa papo. Kielelezo Na.7.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hilo.

Kielelezo Na. 7.2


7.	(i) <u>Kuchora (Uwezo wa kuchora).</u> - Hapa mwalimu atawera kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia
	(ii) <u>Uwezo wa kuchanga (Kuchanga)</u> - Kama mwalimu anawera kuchanga atawere kufara gue zana salili.
	(iii) <u>Ubunifu wa maandishi</u> - Hapa pia itamzaidi mwalimu kufaragua zana za kufundishia kwa kutumia maandishi salili.
	(iv) <u>Kuminda (Uwezo wa kuminda).</u> - Hapa i stadi kumfanya mwalimu awere kuminda vili papo kwa papo na kufanya tika kibare kama halisio.

Kielelezo Na. 7.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeveza kufafanua stadi anazotakiwa kuwanazo mwalimu wa somo la Haiba na Michezo ili kumwezesha kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia papo kwa papo.

2.1.8 Swali la 8: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali la 8 lilitoka katika mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia. Swali lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b). Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kufafanua dhana ya nyenzo za kufundishia, na katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kuainisha makundi ya zana zinazoweza kutumika katika kufundishia somo la Haiba na Michezo. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walifanya swali hili. Kati ya hao, Watahiniwa 696 (14.4%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 36 (0.7%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambaao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 4,111 (84.9%) walipata alama kati ya 3 hadi 4 ambaao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifaalu swali hili kwa kiwango kizuri kutokana na watahiniwa 4,147 (85.6%) kupata alama

kati ya 2 hadi 4 ambazo ndizo alama zilizowawezesha kufaulu swali hili



Chati Na. 8: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 8

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu wa dhana ya nyenzo za kufundishia na makundi ya zana zinazoweza kutumika katika kufundishia somo la Haiba na Michezo. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliweza kujibu vizuri kutohana na kuelewa matakwa ya swali, na kuwa na uelewa mzuri wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa mada ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia. Watahiniwa waliweza kufafanua dhana ya nyenzo za kufundishia na kuainisha makundi ya zana zinazoweza kutumika katika kufundishia somo la Haiba na Michezo kama vile, zana maono, zana masikizi-maono na zana masikizi kwa ufasaha. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote.

Kielelezo Na. 8.1

	<p>8a) Nyenzo za kufundishia; lizi ni vifaa mbalimbali au zana ouato ritemuia kuvalamu bilita rofishe fendo zinzo la kufundishia na ujifunzoj, dorasani, kwa enfanzi mbabu, nipiwa, picha, vroweni, filimbi entelezi, ne vifaa hili ulelo idhilia wo Somo la haiba na michezo</p>
b)	<p>ii) y Zana lugano; lizi ni zana zinzo tunzia ujifunzo wa era ujafanu yaani muche ili kujifunzo ujifunzo wa zana lizi ui U - Pidha</p> <ul style="list-style-type: none"> - Ramani - nipiwa - chapi - karidi
ii)	<p>ii) y Zana mawilezi; lizi ni zana zinzo tunzia ujifunzo wa fahamu wa kuainishi kuhitaji wa kujifunzo toarifa mbalimbali kama mfano - Ngoma</p> <ul style="list-style-type: none"> - fitmibi - Pidha - teteji rekoda
iii)	<p>iii) y Zana basikiri ngoro; lizi ui aina ya zana amba zo kufunzo ujilango yote yo ujafanu yaani kuosibilia na leonano. Kufanya - running</p> <ul style="list-style-type: none"> - lempanga - Siuu - Shema -

Kielelezo Na. 8.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyezeza kufafanua dhana ya nyenzo za kufundishia pamoja na kuainisha makundi ya zana zinazoweza kutumika katika kufundishia somo la Haiba na Michezo.

Licha ya watahiniwa wengi kufanya vizuri, watahiniwa 696 (14.4%) walipata ufaulu hafifu katika swalii hili. Ufaulu huu unahuishwa na sababu mbalimbali kama vile, baadhi ya watahiniwa kutokuelewa matakwa ya swalii na kutoa majibu yasiyo sahihi Kwa mfano, kutaja aina ya zana za kufundishia badala ya makundi ya zana za kufundishia. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetaja aina ya zana zinazoweza

kutumika katika kufundishia na kujifunzia somo la Haiba na Michezo badala ya kuainisha makundi ya zana kama matakwa ya swali yalivyoelekeza.


Kielelezo Na. 8.2

7.	i/ Afahamu umri na uelenzi wa walengwazi. ii/ Azingatia maandishi amayo fundishia. iii/ Maizingira aliyo nazo. iv/ Mpangilio wa clarase lake.
----	--

Kielelezo Na. 8.2: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyechanganya dhana ya makundi ya zana za kufundishia na aina ya zana za kufundishia na hivyo kutopata alama zozote.

2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Ufundishaji, wa Somo la Haiba na Michezo.

Swali la 9 lilitoka katika mada ya Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo. Swali lililenga kupima maarifa ya watahiniwa katika uundaji wa tini za somo kutokana na vyanzo mbalimbali. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kubainisha vyanzo vinne vinavyo mwezesha mwalimu kuandaa tini za somo. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walifanya swali hili. Kati ya watahiniwa hao, watahiniwa 1,064 (22.0%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 1,552 (32.0%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 2,227 (46.0%) walipata alama kati ya 3 hadi 4 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifaulu swali hili kwa kiwango kizuri kutokana na watahiniwa 3,779 (78.0%) kupata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ndizo alama zilizowawezesha kufaulu swali hili.



Chati Na. 9: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swalii la 9

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swalii hili unaonyesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu wa vyanzo vinne vinavyo mwezesha mwalimu kuandaa tini za somo. Kufaulu kwa watahiniwa kulitokana na kuelewa matakwa ya swalii, na kuwa na maarifa kuhusu vyanzo vinavyomwezesha mwalimu kuandaa tini za somo la Haiba na Michezo. Watahiniwa waliweza kubainisha kwa ufasaha vyanzo vinne vinavyomwezesha mwalimu kuandaa tini za somo ambavyo ni muhtasari, vitabu vya ziada na marejeo ya machapisho mbalimbali. Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swalii hilo na kupata alama zote.

Kielelezo Na. 9.1

o9. Kwa kingi maelekei Yaliyomo kati kati
Somo/Mada busilek
Muhtasari wa Somo busilek hums
acidia mwalimu kipata Vitabu Mbinu
cas mengine fa anayohitaji Mwalimu
busilek.
Vitabu vya zile; humsacidia mwele
kipata maelekei lingamfu ha yale
Yaliyomo kati kati kipata che kieku
Marejeo fa machapisho Mbalmabali
Humsacidia mwalimu kijis ni ixa
Kiasi gani auanizieza kipatia kungo
liliukusudina iantka Ufuncheshaji ny
ujifunzeji :

Kielelezo Na. 9.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kujibu swalii hili kwa ufasaha na kupata alama zote.

Aidha, watahiniwa 1,064 (22.0%) walipata ufaulu hafifu katika swali hili kutokana na sababu mbalimbali kama vile baadhi ya watahiniwa kutokuelewa matakwa ya swali na kutoa majibu yasiyo sahihi na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Kwa mfano, wapo baadhi ya watahiniwa walioandika malengo ya tini za somo badala ya vyanzo vya kuandalia tini za somo kama yalivyokuwa maelekezo katika swali. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeleza sababu za kuandaa tini za somo badala ya kuainisha nyenzo zinazoweza kumsaidia wakati wa kuandaa tini.


Kielelezo Na. 9.2

9	D	Lengo la kuandaa tini s. Kiwepo na kitu kuna Chuo elozewa katika tini hiyo ingizandatini?
10	D	Kiwepo na wahitaji vitabu? Wahitaji ni wale wanastaka kupata mara kufikia, tini hiyo
11	D	Kiwepo na ukabu vi vitabu? kubainish na upunguhi wa vitabu maraliku anawez kuandaa tini kiz kubu ya vitabu

Kielelezo Na. 9.2: Kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali na kushindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

2.1.10 Swali la 10: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali la 10 lilitoka katika mada ya Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo. Katika swali hilo Mtahiniwa alitakiwa kubainisha vipengele vinne vilivyopo kwenye shajara ya somo la Haiba na Michezo. Jumla ya watahiniwa 4,843 (100%) walifanya swali hili. Kati ya hao, watahiniwa 915 (18.9%) walipata alama kati ya 0 na 1.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 1,765 (36.4%) walipata alama kati ya 2 na 2.5 ambaao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 2,163 (44.7%) walipata alama kati ya 3 hadi 4 ambaao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifa kwa kiwango kizuri swali hili kutokana na watahiniwa 3,928 (81.1%) kupata alama kati ya 2 hadi 4 ambazo ndizo zilizowawezesha kufaulu swali hili.



Chati Na. 10: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 10

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonyesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu wa vipengele vilivyomo kwenye shajara ya somo la Haiba na Michezo. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulitokana na kuelewa matakwa ya swali, na kuweza kubainisha kwa ufasaha vipengele vinane vya shajara ya somo la Haiba na Michezo. Pia, watahiniwa walionesha kuwa na maarifa yaliyotarajiwa kwa kutoa majibu yaliyokusudiwa. kama vile, mada kuu, mada ndogo, dhana iliyo tumika, tarehe ya kuanza mada, tarehe ya kumaliza mada, sahihi ya mkuu wa idara, sahihi ya mkuu wa shule, sahihi ya mwalimu wa somo Kelelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote.

Kielelezo Na. 10.1

10.	<ul style="list-style-type: none"> i) Mada kuu ii) Mada ndogo iii) Tarehe iliyo apozia kufundisha mada hiyo iv) Tarehe ya kumaliza kufundisha ma da hiyo. v) Sahihi ya mwalimu wa somo vi) Sahihi ya mkuu wa idara ya somo vii) Sahihi ya mwalimu mkuu. viii) Maoni
-----	--

Kielelezo Na. 10.1: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama zote.

Pamoja na ufaulu huu mzuri, watahiniwa 915 (18.9%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu katika swali hilo. Ufaulu huu hafifu ulitokana na sababu mbalimbali kama vile, baadhi ya watahiniwa kutotaja vipengele vyote vinane vilivyopo katika shajara ya somo ili kukidhi matakwa ya swali, kwani wako watahiniwa waliotaja vipengele vinne, vitano, vitatu na hata viwili na baadhi ya watahiniwa kuonesha uelewa finyu wa nyaraka anazotakiwa kutumia mwalimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kama vile, shajara. Kwa mfano, wapo watahiniwa waliobainisha zana za upimaji badala ya vipengele vya shajara ya somo. Kielelezo Na.10.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeorodhesha zana chache za upimaji badala ya kuorodhesha vipengele vya shajara.

Kielelezo Na. 10.2

10	i/ Mkoza wa kazi	
ii/ Itoaji		
iii/ Gedwali		
iv/		

Kielelezo Na. 10.2: Kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu ya siyo sahihi.


2.2 SEHEMU B

Sehemu B ya mtihani wa Somo la Haiba na Michezo ilikuwa na jumla ya maswali 6 ya insha. Kila swali katika sehemu hiyo lilikuwa na jumla ya alama kumi na tano (15). Mtahiniwa alitakiwa kuchagua maswali manne kati ya maswali yote sita. Kufaulu kwa watahiniwa katika sehemu hii kuligawanywa katika makundi matatu kulingana na alama walizopata watahiniwa. Watahiniwa waliopata alama kati ya 0 hadi 5.5 walihesabika kufaulu kwa kiwango hafifu katika swali husika. Watahiniwa walihesabika kufaulu kwa kiwango cha wastani iwapo walipata alama kati ya 6 hadi 10 na watahiniwa waliopata kati ya alama 10.5 hadi 15 walihesabika kufaulu kwa kiwango kizuri.

2.2.1 Swali 11: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo

Swali la 11 lilitoka katika mada ya Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Haiba na Michezo. Swali lililenga kupima nyanja ya matumizi kwa lengo la kutaka kujua kama watahiniwa wanaweza kutumia maarifa waliyoyapata katika kupambanua faida za kuzingatia sheria na kanuni wakati wa kucheza mchezo wowote. Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kufafanua faida za

kuzingatia sheria wakati wa mchezo wowote kwa kutumia hoja tano. Jumla ya watahiniwa 2,661 sawa na asilimia 54.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani wa somo la Haiba na Michezo walifanya swali hili. Kati ya hao, watahiniwa 09 (0.3%) walipata alama kati ya 0 na 5.5 ambaao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 1,673 (62.9%) walipata alama kati ya 6 hadi 10 ambaao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 979 (36.8%) walipata kati ya alama 10.5 hadi 15 ambaao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifaulu swali hilo kutokana na watahiniwa 2,652 (99.7%) kupata alama kati ya 6 hadi 15 ambazo ndizo zilizowawezesha kufaulu swali hili. Chati Na. 11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.



Chati Na. 11: Inaonesha kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 11

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ufahamu wa faida za kuzingatia sheria wakati wa kucheza mchezo wowote ambazo ni pamoja na kukuza vipaji vya wachezaji, kujenga ushirikiano kati ya wachezaji na kuepusha ajali zinazoweza kutokea. Watahiniwa walifaulu swali hili kutokana na kuelewa matakwa ya swali, na kuweza kujibu swali kwa ufasaha. Watahiniwa waliweza kufafanua kwa ufasaha faida za kuzingatia sheria wakati wa kucheza mchezo wowote. Kielelezo Na.11.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

Kielelezo Na. 11.1

II Sheria za mchezo ni kanuni na taratibu za kimichezo amba za mchezoji anapaswa kufuata ili kuwera kuchera mchezo hufika. Mfano mpira wa miguu, mpira wa nyaru, jumastiki, Michero Sabili mchezo ya asili. Mchezo woso te unapocherzwa hauza budi kuzingatia taratibu na sleria zikizo wekiwa ili mchezo huo uweza kueleweka. Zifuatazo ni brachii ya faida za kuizingatia Shenz Walkati wa kuchera mchezo woso oto.

